NAFASI YA TAASISI ZA KIDINI KATIKA KUFANIKISHA UCHAGUZI WA AMANI NA UADILIFU 2015 ZANZIBAR

NA

SHEIKH ABDULLA TALIB ABDULLA

Mada iliyoandaliwa kwa ajili ya Semina ya Kuhamasisha Viongozi wa Dini ya Kiislamu katika Kusimamia Amani wakati wa Uchaguzi Mkuu wa 2015 Zanzibar iliyoandaliwa na UKUEM na JUMAZA kwa kushirikiana na Global Network of Religion for Children

MEI 20, 2015

UTANGULIZI

Mizozo inayofungamana na uchaguzi ni moja ya vitisho vikubwa vinavyohatarisha demokrasia, uthabiti wa kisiasa na maendeleeo ya kijamii na kiuchumi katika visiwa wa Zanzibar. Historia ya kisiasa Zanzibar imesajili matukio mengi ya uvunjifu wa amani na kufanyiana fujo na mara nyingi hufungamana na siasa za vyama vingi hususan katika uchaguzi.

Harakati za kupigania uhuru Zanzibar zilianza mnamo miaka ya hamsini. Chaguzi zilifanyika katika miaka ya 1957, Januari 1961, Juni 1961 and Julai 1963. Katika chaguzi zote hizo vyama vya siasa vilishindana na kupelekea mivutano, uhasama na fujo (Mpangala, 2006). Wanahistoria wamebainisha wazi kuwa dini ilitumika sana kufikisha ujumbe wa kisiasa katika harakati hizo za kupigania uhuru. Mara nyingi nususi na walinganiaji zilitumika kutilia nguvu na kuhamasisha malengo na agenda za kisiasa (Ziddy, 2007).

Baada ya Mapinduzi vyama vyote vya siasa vilifutwa na kubaki na chama kimoja tu cha ASP. Zanzibar iliungana na Tanganyika April 1964 na kufanya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Februari 1977 ASP iliungana na TANU kuunda CCM. Wakati wa utawala wa Chama kimoja chaguzi za Amani zilizofanyika Oktoba 1985 na 1990.

Tanzania iliporejesha tena mfumo wa vyama vingi katika mwaka 1992, changamoto zikajitokeza kwa taasisi nyingi zenye dhamana na wapiga mbiu wa Uchaguzi. Chaguzi za mwaka 1995 na 2000 ziligubikwa na fujo na zikasemwa vibaya na waangalizi wengi wa ndani na nje. (Maliyamkono, 2000). Fujo zilizotokea tarehe 26 and 27 Januari 2001,zilipelekea zaidi ya watu 31 wasio na hatia kupoteza maisha, kiasi cha watu 200 kuwekwa kizuwizini na kushtakiwa kwa makosa mbali mbali, matukio ya kupigwa, kuteswa, kuporwa na kubakwa yaliripotiwa kufanyika. Aidha zaidi ya watu 2000 kutoka Pemba walikimbilia Mombasa – Kenya na kuigeuza tatizo kutoka pahala pa kupokea wakimbizi na kuwa nchi inayokimbiwa. Matukio mengi ya kuhangaishwa, unyanyapaa wa kisiasa, ubaguzi, vitisho, maneo na matendo ya kukashifiana yalienea kabla, wakati na baada ya chaguzi. (Oloka- Onyango na Nassal, 2003). Sababu kubwa ya fujo katika chaguzi za Zanzibar zilikuwa ni pamoja na baadhi ya mapungufu katika mchakato wa kuendesha Uchaguzi na kiwango kikubwa cha kutokuaminiana kati ya vyama vya CCM na CUF.

Uchaguzi wa vyama vingi ni utaratibu wa kidemokrasia unaokusudia kuwawezesha watu kuchagua viongozi wa Serikali na wajumbe wa mabaraza ya kutunga sheria. Kwa hivyo matokeo ya uchaguzi huru na wa uadilifu yanaonyesha sura halisi ya maamuzi ya wananchi (Ramadhan, 1998).Ili uchaguzi uwe wa amani, uhuru na uadilifu utahitaji wadau wote washirikiane katika hatua na taratibu zote za uchaguzi. Mkazo usiwe wakati wa kuhesabu kura na kutangaza

washindi tu lakini uanzie tokea maandalizi ya uchaguzi, wakati wa uchaguzi na baada ya Uchaguzi.

Wadau wote wa uchaguzi wakiwemo Tume za Uchaguzi, vyombo vya dola, vyama vya siasa, wagombea na mawakala wao, vyombo vya habari, waangalizi, watathmini, asasi za kiraia na wapiga kura wana dhamana tofauti katika kushajiisha uchaguzi huru na wa haki. Azma yao ya kweli katika kutetea haki na uadilifu, matumizi ya njia sahihi na taratibu zilizowekwa, na kushiriki katika mchakato mzima wakiwa na uvumilivu na ustaarabu ni masharti muhimu ya kufanyika kwa uchaguzi huru, wa haki na wa amani. Uangalizi, tathmini na juhudi za kujenga amani na uadilifu zinahitajika katika hatua zote tatu za uchaguzi. Hatua hizo ni kama ifuatavyo:-

1. **Kabla ya Uchaguzi:** unaokusanya kukata majimbo, kujiandikisha katika daftari, usajili wa vyama vya siasa, kutangaza wagombea, Matumizi ya rasilimali za Umma, matumizi ya vyombo vya habari, taratibu za kampeni na kutoa elimu ya kura na uraia.
2. **Wakati wa Uchaguzi:** kunakusanya kuhamasisha ushiriki mkubwa kwa kuijenga jamii kujiamini, kuweka uwazi na uwajibikaji. Aidha kupiga kura.
3. **Baada ya Uchaguzi**: kunakusanya kuhesabu kura, kutoa matokeo, kukubali matokeo, kufanya mapitio baada ya uchaguzi na kusuluhisha sitofahamu na migongano.

Zanzibar mara nyingi hufanyika chaguzi mbili kwa pamoja. Uchaguzi mkuu wa Zazibar unaosimamiwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) kwa kuchagua Rais wa Zanzibar, Wawakilishi na madiwani. Wazanzibai pia huchagua Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Wabunge katika uchaguzi unaosimamiwa naTume ya Uchaguzi ya Taifa (NEC).

NAFASI YA DINI KATIKA KUHAKIKISHA UCHAGUZI WA HAKI NA UADILIFU

Mizozo ya kisiasa mara nyingi husababishwa na matatizo ya kutokufanyika haki na uadilifu au kudhani kuwa haki haikutendeka kunakosababishwa na pande zinazoshindana. Mara nyingi kazi inayohitajika ni kubadilisha mifumo na taratibu zinazopelekea kukosekana usawa na uadilifu. Aidha mahusiano na mitazamo miongoni mwa pande zinazozozana yanapaswa kujengwa katika kuwezeshana, uadilifu, amani, kusameheana, kujaliana, kutambuana na utenganifu (Fisher et al, 2005). Zaidi ya hayo Umoja na maslahi ya Taifa vipiwe kipaumbele zaidi.

Dini ina misingi muhimu inayoweza kutumika katika kujenga au kuvunja amani. Hii ni kutokana na athari zake katika kujenga tabia, mitizamo na utambulisho. Aidha kuna uhusiano mkubwa wa kinadharia baina ya dini na uchaguzi wa amani na uadilifu. Uchaguzi wa amani unatokea kwa kuwepo uadilifu, kufuatwa vyema taratibu na miongozo katika mchakato wote, ushirikishwaji wa pande zinazohusika kwa mujibu wa matakwa ya kisheria, kutolewa elimu ya kutosha ya uraia na kura, uwazi (transparence), uwajibikaji na kuyakubali matokeo.Yanapofanyika haya mategemeo ni kufanyika uchaguzi huru na wa haki na hivyo mategemeo makubwa ni kuwa wa

Amani. Dini kwa upande wake inatoa mafunzo ya kiroho, upatanifu, uvumilivu, ushirikiano, kujitolea katika kujenga amani, usuhuba na kuathiri katika utoaji wa maamuzi. Ili dini iweze kudhibiti migogoro, kujenga amani, maridhiano na kuondosha kila aina ya fujo, taasisi za dini zitapaswa kujua taratibu zinazotawala Chaguzi kuu na mipaka yao.

Taasisi za dini zinaweza kushiriki kwa namna tofauti katika kujenga jamii ishiriki katika hatua zote za Uchaguzi na kupiga kura kwa njia za amani. Dua, Mafunzo ya kidini na kulinganiana katika tabia njema na kukumbushana kila siku na kila wakati kunasaidia sana kujenga jamii. Taasisi za dini zinaweza kushiriki kila mwanachama pekee, au kitaasisi au kwa makundi. Upo umuhimu wa kuwa na sehemu ya kuratibu shughuli hizo. Kuna msemo usemao "*anaekwenda peke yake huenda haraka lakini wengi wakienda pamoja hufika mbali".* Aidha tusipopanga ni kupanga kuwa tusifanikiwe.

Kufanya kazi kwa pamoja kutawawezesha kutumia vizuri rasili mali na watu ikiwemo taasisi zenye athari kwenye vyombo vya Serikali, Kutokuelemea katika vyama maalum, walinganiaji wenye mvuto, vyombo vya habari, makundi yenye uwezo wa kukusanya watu wengi, makundi yenye uzoefu na uchaguzi, ulinganiaji katika ngazi za chini na ngazi za kitaifa.

Katika hatua ya kabla ya Uchaguzi taasisi za dini zinaweza kushiriki kikamilifu katika matumizi ya vyombo vya habari na utoaji wa elimu ya kura na uraia. Kazi ya kukata majimbo ni ya ZEC tu kwa mujibu wa Sheria namba. 11 ya 1984. Sheria hiyo pia inakataza taasisi za dini kushiriki katika kampeni. Aidha, taasisi za dini hazitakiwa kujiunga au kuunda Chama cha Siasa kama ilivyobainishwa na sheria namba 5 ya 1992 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Taasisi za dini zinapaswa kushiriki katika kufanikisha uchaguzi wa Amani na uadilifu kwa sababu:-

1. Kufanya kazi ya kujenga Amani ni kutekeleza dhamana ya dini. Uislamu ni amani, maamkizi yao ni amani, marejeo yao siku ya kiama ni nyumba ya amani, Jee kukiwa hakuna amani tutatekeleza majukumu ya kidini. Amesema Allah Mtukufu : ((Na wale waliochukua juhudi kwa ajili yetu basi tutawaongoza katika njia zetu)) Ankabuut 29:68. Mtume SAW amesema: *"Nyote ni wachunga na kila mchunga ataulizwa kuhusu kile alichokichunga…"*
2. Uislamu una misingi inayojenga jamii iliyo na umoja. Ni dini inayosisitiza uadilifu, uvumilivu, maridhiano, maelewano, upendo, heshima, umoja, msamaha na kutii hukmu ya Allah kwa lengo la kufikia amani ya kweli duniani na akhera. Pia inawataka waumini wake waitakidi kadhaa na kadari.
3. Dini ina watendaji wengi walio katika ngazi zote, na utendaj wake hauhitaji gharama kubwa. Hivyo uzoefu na matarajio ni kufanya vizuri zaidi. Wadau wa uchaguzi ni waumini wa dini hivyo wanahudhuria na kusikiliza khutuba za kidini na shughuli za kidini ambazo pia huwakusanya wafuasi na mashabiki wa vyama vyote.

4. Misaada kutoka taasisi za kidini za nje ya Zanzibar. Viongozi wengi wa kidini walio nje ya Zanzibar huwa hawaridhishwi na mivutano ya kisisasa ya Zanzibar na huwa tayari kushirikiana na wazanzibari katika kujenga amani, kutengeneza amani, kukinga fujo kwa njia mbali mbali ikiwemo kusaidia shughuli zinazofanyika na kutoa uzoefu wao bali hata kushiriki binafsi. ((Na saidianeni katika kufanya wema na kumcha Mungu wala msisaidiane katika madhambi na uadui)) Al- Maida (5):48.
5. Mila, ada na desturi za Zanzibar kwa kiasi kikubwa zimejengeka kwa utamaduni wa Kiislamu. Hata maziko na harusi zina nafasi katik akujenga mapenzi na mashirikiano na kupiga vita uadui. Mwenyezi Mungu anasema ((Hakika Allah habadilishi (neema) aliyowaneemesha watu mpaka wayabadilishe yaliyo katika nafsi zao)) (Raad (13):11);
6. Hali halisi ya ulimwengu na athari zinazotokea katika nchi za wenzetu, zinalazimisha kwa mwenye akili kuhangaikia amani kwa thamani yoyote. Hivyo kila mmoja anapaswa kushirikiana na kila mwenye nia, azma na lengo hilo ili kuchangiana nguvu. Amesema Mtume SAW “Hekma ni kitu kilichompotea Muislamu hivyo popote atakapoikuta yeye ndie mwenye haki zaidi nayo”.

In kufikia lengo hilo taasisi za dini zinaweza kutumia mikakati ifuatayo:-

1. Matumizi mazuri ya nyumba za ibada na maeneo ya kidini kama misikiti, zawia. Ijitima, mihadhara kwa kuwa daraja la kuwaunganisha watu, kutoa nasaha na sio kujenga uadui na kufarikisha.
2. Matumizi mazuri ya aya, hadithi, athari, nukuu za kihistoria na hekma nyenginezo. Nasi (nukuu) moja yaweza kutumika kujenga jamii au kuivunja na kuleta maangamizi kwa kutegemea tafsili iliyotolewa. Elimu ni dhamana ambayo intakiwa ibainishwe kwa ukweli. Imamu Ibnul Qayim amewaita wenye elimu kuwa ni “*Wenye kutia saini kwa niaba ya Allah*”. Amesema SAW “Muislamu ni yule ambae wame salimika waislamu wenzake na shari ya mkono wake na ulimi wake”
3. Kila muislamu anatakiwa kuijua, kuilinda na kuihifadhi misingi mitano ambayo dini, nafsi, mali, heshima na kizazi *(Dharuuratul khamsa)*. Amesema Mtukufu ((kwa hakika tumewakirimu (tuhewatukuza) wanadamu)) (Israa (17):70). Haki hizi haziwezi kutekelezeka ipasavyo iwapo kutakuwa na fojo na kutokuaminiana kukubwa.
4. Uislamu unalingania uadilifu kwa gharama yoyote ile. Hii ni kwa sababu bila ya uadilifu amani ya kweli inakuwa ni ndoto kupatikana. Amesema Mtukufu: ((Enyi mlioamini kuweni wasimamizi wa uadilifu, wenye kutekeleza ushahidi kwa ajili ya Allah hata kama ni kinyume na maslahi ya nafsi zenu, au wazazi wenu au jamaa zenu wa karibu. Akiwa ni tajiri (mwenye nguvu na uwezo) au fakiri (mnyonge au vyovyote atakavyokuwa mwenye kutolewa ushahidi) basi Allah ni ana haki zaidi kuliko wao. Wala msifuate matamanio ya nafsi (mkapendelea) na kuacha uadilifu. Na kama mkiupotoa ushahidi au mkapuuza

(kwa kutoutekeleza au kuuficha) basi Allah ni Mjuzi (wa matendo yenu) na Atawalipa kwayo)) (Nisaa (4):135).

5. Kwa kuzingatia uhalisia wa uchaguzi, taasisi za kidini zinapaswa kutumia mbinu na taratibu za kidini na nyenginezo katika kulingania uchaguzi wa amani. Wasijikite katika nyanja na semina za kidini tu bali washirikiane na wadau wote wa uchaguzi katika semina, mikutano, makongamano, mashauriano na mikakati bila ya kukiuka maadili yao ya kidini. Hali hii itawafanya wadau na watu wengi zaidi kunufaika na hekma za kidini. Hivyo pamoja na aya na hadithi taasisi za dini ziweze kujenge hoja za kimantiki na kutumia mifano halisi ya nyakati za tulizonazo katika harakati zao za kuzuwia fujo, kujenga na kufanya amani. Wawe weledi wa kusisitiza misingi ya utawala bora ambayo inafahamika na wadau wengi na wawe tayari kujifunza kwa wataalamu wa nyanja hizo ili wajuwe lugha na mbinu za wengine wenye lengo moja.
6. Kwa kushirikiana na wanasheria, wapitie sheria, kanuni, taratibu na miongozo inayotawalia mabo ya uchaguzi ili kubaini vipengele na mabo ambayo hayafahamiki vyema, yana utata au kuzikwazwa taasisi za kidini katika shughuli zao za kulingania uchaguzi huru na wa uadilifu.
7. Kujenga mazingira bora yatakayozifanya taasisi dini kuwa na wawakilishi wenye sifa katika shughuli zao za kujenga amani, kuwe na uwazi, uwajibikaji na kushikamana na utawala bora ikiwemo kujiepusha nakukemea kwa nguvu zote rushwa. Ili kulifanya hili kwa umakini na umadhubuti taasisi za dini zinaweza kujenga wenza (*partnership)* na taasisi nyengine za nje na ndani au hata za imani nyengine.
8. Kwa kuzingatia kuwa wanaharakati wengi wamekuwa na mikakati na program maalum zilizolengwa kwa wanawake, taasisi za dini ni vyema pia zikaandaa taratibu maalum za kulifika kundi hili ambalo ndio kubwa na linaloonekana ni rahisi kuliteka.

HITIMISHO

Zanzibar ni nchi ndogo yenye watu wachache ambao wanamchangayiko na ujamaa wa karibu. Msiba mdogo unapotokea ni nadra kukuta mtu hakuguswa na msiba huo binafsi yake au jamaa zake, wakwe marafiki na kadhalika. Hivyo, tekelezeni wajibu wenu kikamilifu ili uchaguzi uweze kufanyika katika misingi ya uhuru, uwazi, haki, amani na utulivu.

- Walinga nieni waumini na watu wote kuhakikisha kwamba, wanajitahidi kutekeleza wajibu wao, ili uchaguzi uweze kufanyika katika misingi ya uhuru, uwazi, haki, amani na utulivu.
- Katiba inabainisha wazi kwamba Serikali haina dini, lakini wananchi wana dini na imani zao zinazopaswa kulindwa na kuheshimiwa kikatiba pamoja na kusikilizwa kwa makini

wanapotoa maoni yao. Nidhamu na heshima kwa katiba ya nchi ni kielelezo cha uongozi bora na dalili ya misingi ya haki na amani.

- Katiba au sheria inapopindishwa kwa ajili ya kukidhi maslahi ya watu wachache ndani ya Jamii, hapo mizozo, migogoro na fujo huchochewa na hivyo kulitumbukiza katika maafa makubwa. Tuhimize Viongozi wa kisiasa waheshimu na kuthamini Katiba na sheria za nchi. Uongozi unapaswa kujengeka katika msingi wa huduma na wala si kwa ajili ya kutafuta masilahi ya mtu binafsi, familia yake au kundi linalomuunga mkono.
- Tukumb ushe kuwa uongozi ni kwa ajili ya manufaa ya jamii yote, kwa kusimamia kidete kuwalinda na kuwatetea raia, wakaazi na watembezi hata walio dhaifu; ni changamoto ya kuimarisha na kusimamia misingi ya haki na amani; ili kujenga nchi inayojikita katika amani, upendo, maendeleo na mshikamano wa kitaifa na kimataifa.
- Tutanab ahishe wagombea wa nafasi mbali mbali za uchaguzi kuwa wanapaswa kuonesha ukomavu wa kisiasa katika maneno na mtendo yao, ili kujenga demokrasia ya kweli; wabainishe namna watakavyonyanyua maendeleo ya wapiga kurawao na kamwe, matusi, kejeli, kashfa na matumizi ya nguvu visijitokeze wakati wa mchakato mzima wa uchaguzi.
- Kiongozi wa dini awe ni mtu asiedhihirisha mapenzi yake ya katika vyama vya siasa; kwa vile yeye ni kiongozi wa kiroho, mfano bora na jukumu lake la uchungaji linawahusu wote. Hivyo washajiishe waumini kusikiliza sera na kutafakari kwa makini katika kuwachagua viongozi: waadilifu, wa kweli, walio wazi; walio tayari kusimama kidete kulinda, kutetea na kudumisha misingi ya haki, amani, utu, wema na maendeleo ya taifa.
- Kila mwananchi aliyetimiza masharti akapige kura kwa maamuzi yake binafsi, akiwa huru, bila shinikizo la kimaadili, k hali, kisiasa wala kiuchumi.
- Hamasis ha waandaaji, wasimamizi na watazamaji wa uchaguzi kutoka ndani na nje ya nchi, kuhakikisha kwamba, wanajitahidi kutumia rasilimali iliyopo ili uchaguzi uweze kuwa wa wazi, kweli na haki, katika mchakato mzima.
- Chukua juhudi katika kusimama kidete ili amani na utulivu viweze kudumu. Sala na maombi yakithirishwe lakini peke yake haitoshi ni lazima na juhudi ya watu ipatikane.

VIAMBATISHO

Maana ya Baadhi ya Maneno:

Fujo (Violence) inakusudiwa vitendo, maneno, mitazamo, mifumo au miundo ambayo inasababisha maumivu au uharibifu wa viungo au ya kisaikolojia, kijamii au kimazingira na/au kuzuwia watu wengine kutofikia mahitaji yao ya lazima kibinadamu.

Kubadilisha Mzozo (Conflict transformation) ni mchakato wa kushughulikia kwa upana vyanzo vya mizozo ya kijamii na kisiasa kwa lengo la kubadilisha tabia Uhusiano na mitazamo ya pande zinazozozana ili kuzifanya ziwe na hali inayojenga utulivu wa kisiasa na kijamii.

Kufanya Amani (Peace-making) ni taratibu za kuingilia kati katika mzozo ili kumaliza uhasama na kuleta makubaliano ya hiari baina ya pande zinazopingana

Kujenga Amani (Peace building) ni mipango iliyoundwa kushughulikia vyanzo vya migogoro na malalamiko ya zamani; na kukuza haki na utulivu wa muda mrefu.

Maridhiano (**Reconciliation)** ni mchakato mrefu wa kushinda uhasama na kutokuaminiana baina ya watu waliogawanyika

Mzozo ni mahusiano kati ya pande mbili au zaidi zenye au zinazohisi kuwa na malengo yasiyoendana.

Taasisi za dini inakusanya viongozi wa dini, masheikh, wanachuoni, walimu wa dini, Jumuiya za kidini, vyombo vya habari vya kidini na wanaharakati wakidini.

Udhibiti wa migogoro (conflict management) ni mchakato wa kukuza tabia kwendea mabadiliko chanya katika pande zinazohusika katika mgogoro kupitia hatua kadhaa na kwa kufanya kazi kwa pamoja ili kuzuia na kuepuka vurugu siku zijazo

REJEA:

Abdulla, A.T (2009), The Role of Religion in the 2005 General Elections in Zanzibar. A Dissertation Submitted to the Faculty of Arts and Social Sciences in Partial Fulfilment of the Requirements for the Award of the Degree of Master of Arts in Religions. Peace and Conflict Resolutions of the Islamic University in Uganda.

Alger, C. F. (2002). Religion as a Peace Tool. The Global Review of Ethnopolitics of Ohio State University Vol. 1, N0. 4, 94-109.

Ayang, S. G . (1970). A History of Zanzibar. A Study of Constitutional Development (1933-1964). East Africa Literature Bureau, Nairobi.

Fisher, S. et al. (2005). Working with Conflict: Skills and Strategies for Action. Zed-Book publisher, London.

Karume, A. A. (2006). Religion and Peace Building " A Speech delivered by the President of Zanzibar and the Chairman of Revolution Council at the opening ceremony of the General Meeting of Religious Leaders Peace Building Program in Zanzibar at Bwawani Hotel Zanzibar 3rd May 2006.

Maliyamkono, T. L. (Ed.). (2000). The Political Plight of Zanzibar. TEMA Publisher. Dar es Salaam.

Mpangala, G. P. (2006). The Zanzibar conflict: A search for durable solution**.** In Rupiya M. et al. (Eds.). Civil Security Relations in Tanzania: Investigating the Relationship Between the State, Security Services and Civil Society. The Institute for Security Studies Monograph No 128, December 2006.

Oloka-Onyango J. & Nassal, M. (Eds.). (2003). Constitutionalism and Political Stability in Zanzibar: A search for a New Vision : A report of the fact Finding Mission organized under the auspices of Kituo cha Sheria (constitutional center) October 2003 . Published by the Fredich Elbert Stiftung, Dar es Salaam.

Ramadhan, A. S. L. (1998). The Electoral Process in a Multiparty Democracy. In Peter C. M. & Juma I. H. (Eds.). Fundamental Rights and Freedoms in Tanzania. Mkuki na nyota Publishers. Dar es Salaam.

Ziddy I. H et al. (2007). Sources of Religious Conflicts Among Muslims Particularly in Mosques – Zanzibar. Unpublished Research Report organized by the Zanzibar Mufti's Office